لَآاِلٰهَ اِلَّا اللّٰهُ مُحَمَّدٌ رَّسُوْلُ اللّٰهِ

اَدْعِيَّةُ الْقُرْآنِ الْكَرِيْم

# MAOMBI

# YA

# QUR'AN TUKUFU

**SHEIKH MUZAFFAR AHMAD DURRANI**

**MAOMBI YA QUR'AN TUKUFU**

Mwandishi: Sheikh Muzaffar Ahmad Durrani

© Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya
Tanzania

ISBN 9987-8932-1-x

Chapa ya mara ya Kwanza: 2002
Nakala: 5000
Kimeenezwa na:
Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania
P. O. Box 376
Simu: +255-22-2110473
Fax: +255-22-2121744
Dar es Salaam

Kimechapwa na:
Ahmadiyya Printing Press
S.L.P 376
Dar es Salaam.

# YALIYOMO

Utanguliz ............................................................. 6
Mwenyezi Mungu hukubali maombi ..................... 7
1. Ombi kabla ya maombi ................................ 12
2. Dua ya kuongezewa Elimu ............................ 13
3. Maombi kwa ajili ya wazazi ........................... 13
4. Kuomba ghofira yako na ya wazazi wako na ya waaminio na maangamizi ya wadhalimu ........................ 14
5. Dua kwa ajili ya waaminio waliotangulia ........ 15
6. Maombi ya kupata uwezo wa kushukuru ........16
7. Dua wakati wa kupanda merikebu au chombo chochote ..................................... 18
8. Dua ya kupata ufaulu katika mahubiri ............ 19
9. Dua ya kuokolewa katika wasiwasi wa shetani ..................................................... 20
10. Dua ya kuingia katika mkazi mapya na ya kutoka kwa heshima ............................ 21
11. Dua ya kupata msaada wa Mwenyezi Mungu ........................................... 22
12. Dua ya kuomba msamaha na mwisho mwema ........................................... 23
13. Dua ya kuomba ghofira na rehema ya Mwenyezi Mungu ...................................... 25
14. Dua ya kupata nuru kamili na ulinzi wa Mwenyezi Mungu ............................. 27
15. Dua ya kuomba msamaha na msaada dhidi ya makafiri ............................... 27

16. Dua ya kupata subira na nusura
juu ya makafiri ................................................ 29
17. Dua ya kuomba ghofira yako
na ya kaka yako ............................................ 30
18. Dua ya kutokuwa mkiwa ................................ 30
19. Dua ya kutoa mtoto wakfu
wakati bado yuko tumboni ............................. 31
20. Dua ya kuomba kizazi chema ........................ 32
21. Dua kwa ajili ya ahli na watoto ....................... 33
22. Dua kwa ajili ya kusali wewe
na wazao wako ............................................ 34
23. Dua ya kupata amani ya mji na
kuepukana na ibada ya masanamu ............... 35
24. Dua ya kupata riziki ....................................... 35
25. Dua ya kutopotea baada
ya kuongoka .................................................. 36
26. Dua ya kuokolewa katika mji ambao watu
wake ni wadhalimu na kupata msaidizi
kutoka kwa Mwenyezi Mungu ........................ 37
27. Dua ya upambanuo baina
ya haki na batili ............................................. 38
28. Dua ya kuokolewa na watu wadhalimu .......... 38
29. Dua ya kujiepusha na wadhalimu .................. 39
30. Dua ya wokovu katika hila za wapinzani ........ 40
31. Dua ya kuomba ghofira baada ya kukosea .....40
32. Dua ya kuokolewa katika fitina ya
makafiri na wafisadi ...................................... 41

33. Dua ya kuomba msaada wa Mwenyezi
Mungu baada ya kushindwa jambo ............... 43
34. Dua ya maangamio ya makafiri ..................... 44
35. Dua ya kuomba wema katika dunia na Akhera
na kujikinga na adhabu ya moto .................... 45
36. Dua ya ya kupata subira na kifo chema ......... 47
37. Dua ya kuwa mtu mwema, kutajwa
kwa wema na kupata pepo ............................ 47
38. Dua ya kupata wema katika
dunia na Akhera ............................................. 48
39. Dua ya kuepushwa kuomba juu ya
jambo usilo na elimu nalo ............................. 49
40. Dua ya ya kujikinga kwa Mwenyezi Mungu .... 50

**DUA ZA MANABII / WATU WEMA**

1. Dua ya Nabii Ibrahimu 13, 32, 33, 34, 35, 42, 47.
2. Dua ya Nabii Nuhu 14, 18, 21, 22, 23, 43, 44, 49.
3. Dua ya Nabii Suleiman 16
4. Dua ya Nabii Musa 17, 19, 25, 30, 39, 40, 44, 48.
5. Dua ya Nabii Zakaria 30, 32.
6. Dua ya Nabii Isa 35.
7. Dua ya Nabii Shuaib 38.
8. Dua ya Nabii Lut 40, 41.
9. Dua ya Bibi Mariamu 31.
10. Dua ya watu wa Peponi 38.
11. Dua ya watu wa Pango 22.
12. Dua ya watu wa Nabii Mussa 25, 40, 47.

# UTANGULIZI

Mwenyezi Mungu Ametufundisha maombi mbalimbali katika Qur'an Tukufu kwa ajili ya faida yetu. Manabii wa Mwenyezi Mungu na watu wema walikuwa wakiomba kwa maombi haya.

Maulana Muhammad Ishaq Soofi, Amir na Mbashiri Mkuu wa zamani wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya Uganda aliyakusanya maombi haya pamoja na tafsiri mwaka 1969. Sasa ilihitajika kuiboresha kazi hii. Kwa hiyo Maulana Muzaffar Ahmad Durrani, Amir na Mbashiri Mkuu wa Tanzania amepanga taratibu mpya ya maombi pamoja na matamshi yake kwa herufi za Kilatini. Vile vile jina la Mtume anayehusika na dua fulani limeelezwa.

Bw. Abdulrahman M. Ame, Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya Tanzania kwa shauku kubwa amefanya upangaji na uwekaji wake na masahihisho yake kwenye kompyuta.

Mwenyezi Mungu Awasaidie na Awabariki wahusika wote, Amin.

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْم

## MWENYEZI MUNGU HUKUBALI MAOMBI

Mwenyezi Mungu ambaye ni Muumbaji wa ulimwengu wote anao uhusiano wa kudumu na kila Alichokiumba. Uhusiano huo ni wa Muumbaji na viumbe Vyake, na wa Mwabudiwa na watumishi Wake. Basi ni jukumu la kila mtu kuuimarisha uhusiano huo. Mwenyezi Mungu kwa fadhili na hisani zake, anawahurumia watu wake na anawakurubia.

Njia moja ya kuudumisha uhusiano huu ni kumuomba Mwenyezi Mungu. Bali Mwenyezi Mungu Mwenyewe Amehimiza juu ya jambo hili kwamba tusighafilike kumuomba Mwenyezi Mungu. Mtume Mtukufu Muhammad s.a.w. aliamrishwa aseme kwamba:

قُلْ مَا يَعْبَؤُا بِكُمْ رَبِّىْ لَوْلَا دُعَآؤُكُمْ ۝

"Sema: Mola wangu hangewajalini kama si

kuomba kwenu." (25:78).
Yaani Mwenyezi Mungu anaonesha huruma nyingi kwa sababu ya maombi ya watu.

Tena ameeleza kwamba ni Yeye ambaye anakubali maombi ya wenye matatizo. Kasema kwamba:

أَمَّنْ يُجِيبُ الْمُضْطَرَّ إِذَا دَعَاهُ وَيَكْشِفُ السُّوءَ ۝

"Au ni nani anayemjibu aliyedhikika amwombapo na kuondoa dhiki." (27:63).

Yaani ni Mwenyezi Mungu ambaye anakubali maombi yetu na anaondoa matatizo na dhiki zetu. Ni Yeye tu ambaye tunaweza kumkumbuka na kumuomba wakati wa mahitaji yetu. Bali Yeye ametuamrisha kumuomba kwa faida yetu na ametuahidi kwamba atakubali maombi yetu.

Mwenyezi Mungu ametuelezea kupitia Mtume Mtukufu Muhammad s.a.w. masharti ya

kukubalika maombi, amesema kwamba:

وَإِذَا سَأَلَكَ عِبَادِي عَنِّي فَإِنِّي قَرِيبٌ أُجِيبُ دَعْوَةَ الدَّاعِ إِذَا دَعَانِ
فَلْيَسْتَجِيبُوا لِي وَلْيُؤْمِنُوا بِي لَعَلَّهُمْ يَرْشُدُونَ ۝

"Na watu wangu watakopokuuliza juu yangu, basi hakika mimi nipo karibu. Nayaitika maombi ya mwombaji anaponiomba. Basi waniitikie na waniamini ili wapate kuongoka." (2:187).

Katika aya hii Mwenyezi Mungu ametubashiria kwamba Yeye yupo karibu sana na hukubali na hujibu maombi ya watu, wakati wanapomwomba. Lakini kwa ajili ya kukubali maombi ameweka masharti mawili.

1. Watu na waombaji waniitikie Mimi (Allah), yaani watu wafuate amri Zangu na watekeleze wajibu wao kulingana na mafundisho Yangu.

2. Waombaji waniamini Mimi (Allah). Yaani imani yao iwe imara juu ya Mwenyezi Mungu na wasimshirikishe na chochote wala

wasimtegemee yeyote minghairi ya Mwenyezi Mungu. Imani yao iwe ya hali ya juu. Na haya ni masharti mawili na njia sahihi ili wapate kuongoka.

Kisha Mwenyezi Mungu ametufundisha adabu na taratibu za kumwomba amesema kwamba:

وَلَا تَجْهَرْ بِصَلَاتِكَ وَلَا تُخَافِتْ بِهَا وَابْتَغِ بَيْنَ ذَٰلِكَ سَبِيلًا ۝

Wala usiseme dua zako kwa sauti kubwa, wala usiseme kwa sauti ndogo bali ushike njia baina ya hizo." (17:111).

Yaani Mwenyezi Mungu yu karibu na Msikiaji sana. Kwahiyo haina maana kupiga makelele wakati wa kumwomba. Lakini kwa ajili ya kuondoa usingizi na fikra mbalimbali tunafundishwa kuomba kwa sauti ndogo.

Katika kurasa zijazo tunawaletea wasomaji

wetu maombi ya Qur'an Tukufu. Maombi haya mengi ni ya Manabii wa zamani waliyofundishwa na Mwenyezi Mungu kumuomba. Kwa hiyo tumeandika kabla ya dua kwamba dua hii iliombwa na Nabii fulani. Baadhi ya maombi, kwa uchache sana, ni ya watu wema wengine. Na maombi mengine ni yale aliyofundishwa Mtume Mtukufu Muhammad s.a.w.

Mwenyezi Mungu atujaalie kumuomba Muumbaji wetu na kumshukuru juu ya aliyotusaidia katika mambo yote. Amin.

Sheikh Muzaffar Ahmad Durrani
Dar es Salaam
6.3.2002

## 1. OMBI KABLA YA MAOMBI

بِسۡمِ اللّٰهِ الرَّحۡمٰنِ الرَّحِيۡم ﴿١﴾

اَلۡحَمۡدُ لِلّٰهِ رَبِّ الۡعٰلَمِيۡنَ ﴿٢﴾ الرَّحۡمٰنِ الرَّحِيۡمِ ﴿٣﴾

مٰلِكِ يَوۡمِ الدِّيۡنِ ﴿٤﴾ اِيَّاكَ نَعۡبُدُ وَ اِيَّاكَ نَسۡتَعِيۡنُ ﴿٥﴾

اِهۡدِنَاالصِّرَاطَ الۡمُسۡتَقِيۡمَ ﴿٦﴾ صِرَاطَ الَّذِيۡنَ اَنۡعَمۡتَ عَلَيۡهِم

غَيۡرِ الۡمَغۡضُوۡبِ عَلَيۡهِم وَلَاالضَّآلِّيۡنَ ﴿٧﴾

**Matamshi:**

*Bismillahir Rahmaanir Rahiim. Alhamdulillaahi Rabbil 'Alamiin Arrahmaanir Rahiim. Maaliki yawmid Diin. Iyyaka na'budu waiyyaka nastaiin. Ihdinas Swiraatwalmustaqiim. Swiraatwalladhiina An'amta alaihim ghairil maghdhuubi 'alaihim waladhdhaaliin.*

**Tafsiri:**

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu. Sifa zote njema zinamhusu Mwenyezi Mungu, Mola wa

walimwengu, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu, Mmiliki wa siku ya malipo. Wewe tu twakuabudu, na Wewe tu twakuomba msaada. Utuongoze njia iliyonyooka. Njia ya wale Uliowaneemesha; siyo ya wale walioghadhibikiwa, wala siyo ya wale waliopotea.

## 2. DUA YA KUONGEZEWA ELIMU

رَّبِّ زِدْنِىْ عِلْمًا ۝

***Matamshi:*** *Rabbi zidnii Ilmaa.*

**Tafsiri:** Mola wangu, nizidishie elimu. (20:115)

## 3. MAOMBI KWA AJILI YA WAZAZI

### A. (Dua ya Nabii Ibrahim a.s.)

رَبَّنَا اغْفِرْ لِىْ وِلِوَا لِدَىَّ وَلِلْمُؤْمِنِيْنَ يَوْمَ يَقُوْمُ الْحِسَابُ ۝

***Matamshi:*** *Rabbanaghfirlii waliwaalidayya*

*walilmu'miniina yauma yaquumulhisaab.*

**Tafsiri:** Ee Mola wangu unisamehe mimi na wazazi wangu na wale walioamini siku ya kusimama hesabu. (14:42).

رَّبِّ ارْحَمْهُمَا كَمَا رَبَّيَانِي صَغِيرًا۝

**B.** ***Matamshi:***
*Rabbir hamhumaa kamaa rabbayaani swaghiira.*

**Tafsiri:** Ee Mola wangu uwarehemu hawa wawili (wazazi wangu) kama walivyonilea nilipokuwa mdogo. (17:25).

## 4. KUOMBA GHOFIRA YAKO NA YA WAZAZI NA YA WAAMINIO NA MAANGAMIZO YA WADHALIMU

**(Dua ya Nabii Nuhu a.s.).**

رَّبِّ اغْفِرْ لِي وَلِوَالِدَيَّ وَلِمَنْ دَخَلَ بَيْتِيَ مُؤْمِنًا وَّ لِلْمُؤْمِنِينَ

وَالْمُؤْمِنٰتِ وَ لَا تَزِدِ الظّٰلِمِيْنَ اِلَّا تَبَارًا ۞

***Matamshi:*** *Rabbighfirlii waliwaalidayya waliman dakhala baitiya mu'minan walilmu'miniina walmu'minaati walaa tazidi dhdhaalimiina illa tabaaraa.*

**Tafsiri:** Ee Mola wangu nighofirie mimi na wazazi wangu na wale walioamini miongoni mwa wanaume na wanawake na usiwazidishie wadhalimu ila maangamizo. (71:29).

## 5. DUA KWA AJILI YA WAAMINIO WALIOTANGULIA

رَبَّنَا اغْفِرْ لَنَا وَلِإِ خْوَانِنَا الَّذِيْنَ سَبَقُوْنَا بِالْإِيْمَانِ وَ لَا تَجْعَلْ فِيْ
قُلُوْبِنَا غِلًّا لِّلَّذِيْنَ اٰمَنُوا رَبَّنَآ اِنَّكَ رَئُوفٌ رَّحِيْمٌ ۞

***Matamshi:*** *Rabbanaghfirlanaa wal ikhwaanina lladhiina sabaquuna bil iimaan walaa taj'al fii*

*quluubinaa ghilla lilladhiina aamanu, Rabbanaa innaka Rauufur Rahiim.*

**Tafsiri:** Mola wetu, Utughofiri pamoja na ndugu zetu waliotutangulia katika imani wala Usiweke mafundo katika mioyo yetu kwa walioamini; Mola wetu, hakika Wewe ni Mpole sana. Mwenye rehema. (59:11).

## 6. MAOMBI YA KUPATA UWEZO WA KUSHUKURU

### A. (Dua ya Nabii Suleiman a.s.).

رَّبِّ اَوْزِعْنِىٓ اَنْ اَشْكُرَ نِعْمَتَكَ الَّتِىٓ اَنْعَمْتَ عَلَىَّ وَعَلٰى وَا لِدَىَّ وَاَنْ
اَعْمَلَ صَالِحًا تَرْضٰهُ وَاَدْخِلْنِى بِرَحْمَتِكَ فِى عِبَا دِكَ الصّٰلِحِيْنَ ۝

***Matamshi:*** *Rabbi auz'enii an ashkura ne'matakal latii an'amta 'alayya wa 'alaa waalidayya wa an a'mala swaalihan tardhaahu wa ad'khlinii bi rahmatika fii ibaadikas swalihiin.*

**Tafsiri:** Ee Mola wangu, Unipe nguvu nishukuru neema Zako Ulizonineemesha mimi na wazazi wangu, na nipate kufanya vitendo vizuri vikupendezavyo, na Uniingize kwa rehema Zako katika watumishi Wako wema. (27:20).

**B. (Dua ya Nabii Musa a.s.)**

رَّبِّ اَوْزِعْنِىٓ اَنْ اَشْكُرَ نِعْمَتَكَ الَّتِىٓ اَنْعَمْتَ عَلَىَّ وَعَلٰى وَا لِدَىَّ وَاَنْ
اَعْمَلَ صَالِحًا تَرْضٰهُ وَاَصْلِحْ لِىْ فِىْ ذُرِّيَّتِىْ اِنِّىْ تُبْتُ اِلَيْكَ وَاِنِّىْ مِنَ
الْمُسْلِمِيْنَ ۞

***Matamshi:*** *Rabbi auz'enii an ashkura ne'matakal latii an'amta 'alayya wa 'alaa waalidayya wa an a'mala swaalihan tardhaahu wa aslih lii fii dhurriyyatii innii tubtu ilaika wa innii minal muslimiin.*

**Tafsiri:** Ee Mola wangu, Uniwezeshe nishukuru neema Zako ulizonineemesha mimi na wazazi

wangu, na ili nifanye vitendo vizuri Unavyovipenda, na Ukanifanyie wema katika watoto wangu; kwa yakini ninatubu Kwako; na hakika mimi ni miongoni mwa waliosilimu. (46:16)

## 7. DUA WAKATI WA KUPANDA MERIKEBU AU CHOMBO CHOCHOTE

### A. (Dua ya Nabii Nuhu a.s.)

بِسْمِ اللّٰهِ مَجْرِيهَا وَمُرْسٰهَا اِنَّ رَبِّى لَغَفُوْرٌ رَّحِيْمٌ ۞

***Matamshi:*** *Bismillahi Majreehaa wamursaahaa inna rabbii laghafuurur Rahiim.*

**Tafsiri:** Kwa jina la Mwenyezi Mungu, kuwe kwenda kwake na kusimama kwake, hakika Mola wangu ni Msamehevu sana, Mrehemevu. (11:42).

سُبْحٰنَ الَّذِىْ سَخَّرَ لَنَا هٰذَا وَمَا كُنَّا لَهٗ مُقْرِنِيْنَ ۞ وَاِنَّا اِلٰى رَبِّنَا لَمُنْقَلِبُوْنَ ۞

**B.** ***Matamshi:*** *Subhaanal ladhii sakhkhara lanaa haadhaa wamaa kunnaa lahuu muqriniina wainnaa ilaa rabbinaa lamunqalibuun:*

**Tafsiri:** Atukuzwe yeye aliyetutiishia haya na tusingaliweza kutenda haya wenyewe. Na bila shaka sisi tunarudia kwa Mola wetu.(43:14-15).

## 8. DUA YA KUPATA UFAULU KATIKA MAHUBIRI.

**(Dua ya Nabii Musa a.s.)**

رَّبِّ اشْرَحْ لِي صَدْرِي ۞ وَيَسِّرْ لِيْ اَمْرِي ۞
وَاحْلُلْ عُقْدَةً مِّنْ لِّسَانِيْ ۞ يَفْقَهُوا قَوْلِيْ ۞

***Matamshi:*** *Rabbish rahlii swadrii wayassirlii amrii wahlul ‘uqdatan millisaani yafqahuu qaulii.*

**Tafsiri:** Mola wangu! Unipanulie kifua changu.

Na Unifanyie rahisi kazi yangu. Na ufungue kifungo katika ulimi wangu. Wapate kufahamu kauli yangu. (20:26-29).

## 9. DUA YA KUOKOLEWA KATIKA WASIWASI WA SHETANI

رَّبِّ اَعُوْذُ بِكَ مِنْ هَمَزٰتِ الشَّيٰطِيْنِ ۞
وَ اَعُوْذُ بِكَ رَبِّ اَنْ يَّحْضُرُوْنِ۞

***Matamshi:*** *Rabbi 'auudhubika min hamazaati shshayaatwiin waa'uudhubika rabbi an yyahdhuruun.*

**Tafsiri:** Mola wangu najikinga kwako uniepushe na wasiwasi wa mashetani. Na najikinga Kwako Mola wangu ili wasinihudhurie. (23:98-99).

## 10. DUA YA KUINGIA KATIKA MAKAZI MAPYA NA YA KUTOKA KWA HESHIMA

**A. (Dua ya Nabii Nuhu a.s.)**

رَبِّ اَنْزِلْنِى مُنْزَلًا مُّبٰرَكًا وَّاَنْتَ خَيْرُ الْمُنْزِلِيْنَ ۝

***Matamshi:*** *Rabbi anzilnii Munzalan Mubaarakan wa anta khairul Munziliin.*

**Tafsiri:** Mola wangu uniteremshe uteremsho wenye baraka, maana wewe ni mbora wa wateremshao. (23:30).

رَبِّ اَدْخِلْنِى مُدْخَلَ صِدْقٍ وَّاَخْرِجْنِى مُخْرَجَ صِدْقٍ وَّاجْعَلْ لِّىْ مِنْ لَّدُنْكَ سُلْطٰنًا نَّصِيْرًا ۝

**B. *Matamshi:*** *Rabbi Ad’khilnii mud'khala swidiqin wwa’akhrij'nii mukhraja swidiqin wwaj’allii milladunka sultwanan naswiira.*

**Tafsiri:** Mola wangu uniingize mwingizo mwema, na Unitoe kutoka kwema. Na unipe nguvu kutoka Kwako isaidiayo. (17:81).

## 11. DUA YA KUPATA MSAADA WA MWENYEZI MUNGU

**A. (Dua ya watu wa pango).**

رَبَّنَآ اٰتِنَا مِنۡ لَّدُنۡكَ رَحۡمَةً وَّهَيِّئۡ لَنَا مِنۡ اَمۡرِنَا رَشَدًا ۝

***Matamshi:*** *Rabbanaa aatinaa milladunka rahmatan wwahayyi'i lanaa min amrinaa rashadaa.*

**Tafsiri:** Mola wetu utupe rehema kutoka Kwako na ututengenezee mwongozo katika jambo letu. (18:11).

**B. (Dua ya Nabii Nuhu a.s.).**

اَنِّىۡ مَغۡلُوۡبٌ فَانۡتَصِرۡ ۝

***Matamshi:*** *Annii maghluubun fantaswir.*

**Tafsiri:** Kwa hakika nimeshindwa basi unisaidie. (54:11).

**C. (Dua ya Nabii Nuhu a.s.).**

رَبِّ انْصُرْنِى بِمَا كَذَّبُوْنِ ۝

***Matamshi:*** *Rabbin swurnii bimaa kadhdhabuun.*

**Tafsiri:** Mola wangu unisaidie kwa sababu wamenikadhibisha. (23:27).

## 12. DUA YA KUOMBA MSAMAHA NA MWISHO MWEMA

رَبَّنَآ اِنَّنَا سَمِعْنَا مُنَادِيًا يُّنَادِىْ لِلْاِيْمَانِ اَنْ اٰمِنُوْا بِرَبِّكُمْ فَاٰمَنَّا رَبَّنَا فَاغْفِرْ لَنَا ذُنُوْبَنَا وَكَفِّرْ عَنَّا سَيِّاٰتِنَا وَتَوَفَّنَا مَعَ الْاَبْرَارِ ۝

رَبَّنَا وَاٰتِنَا مَاوَعَدْ تَنَا عَلَى رُسُلِكَ وَلَا تُخْزِنَا يَوْمَ الْقِيٰمَةِ ۗ اِنَّكَ لَاتُخْلِفُ الْمِيْعَادَ ۝

***Matamshi:*** *Rabbanaa Innanaa sami'enaa munaadiyay yunaadii lil iimaani an`aaminuu birabbikum fa`aamannaa - Rabbanaa faghfir lanaa dhunuubanaa wakaffir 'annaa sayyiaatinaa watawaffanaa ma'al'abraar. Rabbanaa wa-aatinaa maa wa'adtanaa 'alaa rusulika walaa tukhzinaa yaumal qiyaamati innaka laa tukhliful mi'aad.*

**Tafsiri:** Mola wetu, hakika tumesikia Mwitaji anayeita kwenye imani ya kwamba mwaminini Mola wenu, kwa hiyo tumeamini. (Kwa hiyo) Mola wetu, Utusamehe madhambi yetu na Utuondolee maovu yetu na wakati wa kifo chetu Utuunganishe pamoja na watu wema. Mola wetu, na Utupe Uliyotuahidi kwa Mitume Wako, wala Usitufedheheshe siku ya Kiyama;

bila shaka Wewe huvunji miadi. (3:194-195).

**B. (Dua ya wachawi waliomwamini Nabii Musa a.s.)**

رَبَّنَآ اَفۡرِغۡ عَلَيۡنَا صَبۡرًا وَّتَوَفَّنَا مُسۡلِمِيۡنَ ۝

***Matamshi:*** *Rabbanaa afrigh alainaa swabran wwa tawaffanaa muslimiin.*

**Tafsiri:** Mola wetu tumiminie subira na utufishe Waislamu (watii) (7:127).

## 13. DUA YA KUOMBA GHOFIRA NA REHEMA YA MWENYEZI MUNGU

**A. (Dua ya Nabii Musa a.s.)**

اَنۡتَ وَلِيُّنَا فَاغۡفِرۡ لَنَا وَارۡحَمۡنَا وَاَنۡتَ خَيۡرُ الۡغٰفِرِيۡنَ ۝

***Matamshi:*** *Anta waliyyunaa faghfirlanaa warhmanaa wa anta khairul ghaafiriin.*

**Tafsiri.** Wewe ndiwe Mlinzi wetu basi tusamehe na Uturehemu, nawe ndiwe Mbora wa kughofiri. (7:156).

رَبَّنَآ اٰمَنَّا فَاغْفِرْ لَنَا وَارْحَمْنَا وَاَنْتَ خَيْرُ الرّٰحِمِيْنَ ۝

**B.** ***Matamshi:*** *Rabbanaa aamannaa faghfir lanaa warhamnaa wa anta khairur Raahimiin.*

**Tafsiri:** Mola wetu tumeamini, basi tusamehe na turehemu nawe ndiwe Mbora wa wanaorehemu (23:110).

رَبِّ اغْفِرْ وَارْحَمْ وَاَنْتَ خَيْرُ الرّٰحِمِيْنَ ۝

**C.** ***Matamshi:*** *Rabbi ghfir warham wa anta khairur Raahimiin:*

**Tafsiri:** Mola wangu samehe na rehemu, nawe ndiwe Mbora wa wanaorehemu (23:119).

## 14. DUA YA KUPATA NURU KAMILI NA GHOFIRA YA MWENYEZI MUNGU

رَبَّنَآ اَتۡمِمۡ لَنَا نُوۡرَنَا وَاغۡفِرۡ لَنَا اِنَّكَ عَلٰى كُلِّ شَىۡءٍ قَدِيۡرٌ ۞

***Matamshi:*** *Rabbanaa Atmim lanaa nuuranaa waghfir lanaa innaka alaa kulli shai'in Qadiir.*

**Tafsiri:** Mola wetu Ututimizie nuru yetu na Utughofirie, hakika wewe ni Mwenye uwezo juu ya kila kitu.(66:9).

## 15. DUA YA KUOMBA MSAMAHA NA MSAADA DHIDI YA MAKAFIRI

رَبَّنَا لَا تُؤَاخِذۡنَآ اِنۡ نَّسِيۡنَآ اَوۡ اَخۡطَاۡنَا رَبَّنَا وَلَا تَحۡمِلۡ عَلَيۡنَا
اِصۡرًا كَمَا حَمَلۡتَهٗ عَلَى الَّذِيۡنَ مِنۡ قَبۡلِنَا رَبَّنَا وَلَا تُحَمِّلۡنَا مَا
لَا طَاقَةَ لَنَا بِهٖ وَاعۡفُ عَنَّا وَاغۡفِرۡ لَنَا وَارۡحَمۡنَا اَنۡتَ مَوۡلٰنَا
فَانۡصُرۡنَا عَلَى الۡقَوۡمِ الۡكٰفِرِيۡنَ ۞

**A.** ***Matamshi:*** *Rabbanaa laa tuaakhidhnaa inna siinaa au akhtwa'naa. Rabbanaa walaa tahmil alainaa iswran kamaa hamaltahuu ‘alalladhiina min qablinaa. Rabbanaa walaa tuhammilnaa maa laa twaaqatalanaa bihi. Wa’fu’annaa waghfirlanaa warhamnaa. Anta maulaanaa fansurnaa alalqaumil kaafiriin.*

**Tafsiri:** Mola wetu, Usitushike kama tukisahau au tukikosa, Mola wetu, na Usitubebeshe mzigo kama Ulivyowabebesha wale waliokuwa kabla yetu. Mola wetu, Usitutwike tusiyoyaweza, na Utusamehe, na Utughofirie, na Uturehemu; Wewe ndiwe mlinzi wetu; basi Utusaidie juu ya watu makafiri. (2:287).

رَبَّنَااغْفِرْ لَنَا ذُنُوبَنَا وَاِسْرَا فَنَا فِىٓ امْرِنَا وَثَبِّتْ اَقْدَامَنَا
وَنْصُرْنَا عَلَى الْقَوْمِ الْكٰفِرِيْنَ ۞

**B.** ***Matamshi:*** *Rabbana gh'firlanaa dhunuubanaa wa israafanaa fii amrinaa wa*

*thabbit aqdaamanaa wanswurnaa alal-qaumil kaafiriin:*

**Tafsiri:** Mola wetu tughofirie madhambi yetu na kupita kwetu kiasi katika mambo yetu na Uimarishe miguu yetu na Utusaidie juu ya watu makafiri.(3:148).

## 16. DUA YA KUPATA SUBIRA NA NUSURA JUU YA MAKAFIRI

رَبَّنَآ اَفۡرِغۡ عَلَيۡنَا صَبۡرًا وَّثَبِّتۡ اَقۡدَامَنَا وَانۡصُرۡنَا عَلَى الۡقَوۡمِ الۡكٰفِرِيۡنَ ۝

***Matamshi:*** *Rabbanaa afrigh 'alainaa swabran wwa thabbit aqdaamanaa wanswurna Alal-qaumil kaafiriin:*

**Tafsiri:** Mola wetu tumiminie subira na Uimarishe miguu yetu na Utusaidie juu ya watu makafiri.(2:251).

**17. DUA YA KUOMBA GHOFIRA YAKO NA YA KAKA YAKO**
**(Dua ya Nabii Musa a.s.)**

رَبِّ اغْفِرْلِيْ وَلِأَخِيْ وَاَدْخِلْنَا فِيْ رَحْمَتِكَ وَاَنْتَ اَرْحَمُ الرّٰحِمِيْنَ ۝

***Matamshi:*** *Rabbi gh'firlii waliakhii wa ad'khilnaa fii rahmatika wa anta Arhamur Raahimiin.*

**Tafsiri:** Mola wangu unisamehe mimi na ndugu yangu, na Utuingize katika rehema zako maana Wewe ndiwe Mrehemevu zaidi kuliko wanaorehemu. (7:152).

**18. DUA YA KUTOKUWA MKIWA**
**(Dua ya Nabii Zakaria a.s.)**

رَبِّ لَاتَذَرْنِيْ فَرْدًا وَّاَنْتَ خَيْرُ الْوٰرِثِيْنَ ۝

***Matamshi:*** *Rabbii laa tadharnii fardan wwa*

*anta khairul waarithiin.*

**Tafsiri:** Mola wangu usiniache peke yangu; na Wewe ndiwe Mbora wa wanaorithi. (21:90).

## 19. DUA YA KUTOA MTOTO WAKFU WAKATI BADO YUKO TUMBONI (Dua ya Bibi Mariamu)

رَبِّ اِنِّىْ نَذَرْتُ لَكَ مَا فِىْ بَطْنِىْ مُحَرَّرًا فَتَقَبَّلْ مِنِّىْ اِنَّكَ اَنْتَ السَّمِيْعُ الْعَلِيْمُ ۝

***Matamshi:*** *Rabbi Innii nadhartu laka maa fii batwnii Muharraran fataqabbal minnii, Innaka antas samiiul 'aliim.*

**Tafsiri:** Mola wangu hakika nimeweka nadhiri Kwako aliyomo tumboni mwangu kuwa wakfu; basi nikubalie. Bila shaka Wewe ndiwe Usikiaye, Ujuaye. (3:36).

**20. DUA YA KUOMBA KIZAZI CHEMA**

**A. (Dua ya Nabii Ibrahim a.s.).**

رَبِّ هَبْ لِيْ مِنَ الصّٰلِحِيْنَ ۞

***Matamshi:*** *Rabbi hab lii minasswaalihiin:*

**Tafsiri:** Mola wangu nipe (mwana) miongoni mwa watendao wema. (37:101).

**B. (Dua ya Nabii Zakaria a.s.)**

رَبِّ هَبْ لِيْ مِنْ لَّدُنْكَ ذُرِّيَّةً طَيِّبَةً اِنَّكَ سَمِيْعُ الدُّعَآءِ

***Matamshi:*** *Rabbi hab lii min ladunka dhurriyyatan twayyibatan Innaka samiiu ddu'aa*

**Tafsiri:** Mola wangu unipe kutoka Kwako wazao wazuri; kwa yakini wewe ndiwe usikiaye maombi. (3:39).

**C. Dua ya Nabii Zakaria a.s.**

هَبْ لِيْ مِنْ لَّدُنْكَ وَلِيًّا

***Matamshi:*** *Hab lii min ladunka waliyyaa.*
Tafsiri: (Mola wangu) Unipe mrithi kutoka Kwako. (19:6).

## 21. DUA KWA AJILI YA AHLI NA WATOTO
### A. (Dua ya Nabii Ibrahim a.s.)

رَبَّنَا وَا جْعَلْنَا مُسْلِمَيْنَ لَكَ وَمِنْ ذُرِّيَّتِنَآ اُمَّةً مُّسْلِمَةً لَّكَ وَاَرِنَا
مَنَاسِكَنَا وَتُبْ عَلَيْنَا اِنَّكَ اَنْتَ التَّوَّابُ الرَّحِيْمُ ۝

***Matamshi:*** *Rabbanaa waj'alnaa muslimaini laka wamin dhurriyyatinaa ummatan mmuslimatan llaka, wa arinaa manaasikanaa watub'alainaa innaka antat tawwaabur Rahiim.*

**Tafsiri:** Ee Mola wetu, Utufanye tuwe wajitupao Kwako, na miongoni mwa wazao wetu pia Uwafanye watu wajitupao Kwako. Na Utuonyeshe njia za ibada yetu na Utuelekee; bila

shaka Wewe ndiwe Mwelekevu, Mrehemevu. (2:129).

رَبَّنَا هَبْ لَنَا مِنْ اَزْوَاجِنَا وَذُرِّيّٰتِنَا قُرَّةَ اَعْيُنٍ وَّجْعَلْنَا لِلْمُتَّقِيْنَ اِمَامًا ۞

**B. *Matamshi:*** *Rabbanaa hab lanaa min az'waajinaa wadhurriyyaatinaa qurrata a'yunin waj'alnaa lilmuttaqiina imaamaa.*

**Tafsiri:** Mola wetu utupe katika wake zetu na watoto wetu yaburudishayo macho, na Utujaalie kuwa viongozi kwa wamchao (Mungu).(25:75).

## 22. DUA KWA AJILI YA KUSALI WEWE NA WAZAO WAKO
**(Dua ya Nabii Ibrahimu a.s.).**

رَبِّ اجْعَلْنِىْ مُقِيْمَ الصَّلٰوةِ وَمِنْ ذُرِّيَّتِى رَبَّنَا وَتَقَبَّلْ دُعَآءِ ۞

***Matamshi:*** *Rabbij'alnii muqiima sswalaati wa min dhurriyyatii. Rabbanaa wa taqabbal du'aa.*

**Tafsiri:** Mola wangu unijaalie niwe msimamisha sala na wazao wangu (pia); Mola wetu na Upokee maombi yangu. (14:42).

## 23. DUA YA KUPATA AMANI YA MJI NA KUJIEPUSHA NA IBADA YA MASANAMU (Dua ya Nabii Ibrahim a.s.)

رَبِّ اجْعَلْ هٰذَا الْبَلَدَ اٰمِنًا وَّاجْنُبْنِيْ وَبَنِيَّ اَنْ نَّعْبُدَ الْاَصْنَامَ ۞

**Matamshi:** *Rabbij'al haadhal balada aaminan wwaj'nubnii wabaniya an na'buda l'aswnaam.*

**Tafsiri:** Mola wangu, Ujaalie mji huu uwe wa amani, na Unitenge mimi na wanangu tusiabudu masanamu. (14:36).

## 24. DUA YA KUPATA RIZIKI (Dua ya Nabii Isa a.s.)

اَللّٰهُمَّ رَبَّنَآ اَنْزِلْ عَلَيْنَا مَآئِدَةً مِّنَ السَّمَآءِ تَكُوْنُ لَنَا عِيْدًا لِّاَوَّلِنَا
وَاٰخِرِنَا وَاٰيَةً مِّنْكَ وَارْزُقْنَا وَاَنْتَ خَيْرُ الرّٰزِقِيْنَ ۞

***Matamshi:*** *Allaahumma Rabbanaa Anzil ‘Alainaa Maaidatan mminassamaai takuunu lanaa 'iiddaliawwalinaa wa aakhirinaa wa aayatan mminka warzuqnaa wa anta khairur Raaziqiin.*

**Tafsiri:** Mola wetu, tuteremshie chakula kutoka mbinguni ili kiwe sikukuu kwa ajili ya wa mwanzo wetu na wa mwisho wetu, na kiwe Ishara itokayo Kwako, na Uturuzuku, kwani Wewe ni Mbora wa wanaoruzuku. (5:115).

## 25. DUA YA KUTOPOTEA BAADA YA KUONGOKA

رَبَّنَا لَا تُزِغْ قُلُوبَنَا بَعْدَ إِذْ هَدَيْتَنَا وَهَبْ لَنَا مِن لَّدُنكَ رَحْمَةً إِنَّكَ أَنتَ الْوَهَّابُ ۝

***Matamshi:*** *Rabbanaa laa tuzigh quluubanaa ba’ada idh hadaitanaa wa hab lanaa milladunka rahmatan, Innaka antal Wahhaab.*

**Tafsiri:** Mola wetu usiipotoshe mioyo yetu baada ya Kutuongoza, na Utupe rehema kutoka Kwako, hakika Wewe ndiwe Mpaji Mkuu.(3:9).

## 26. DUA YA KUOKOLEWA KATIKA MJI AMBAO WATU WAKE NI WADHALIMU NA KUPATA MSAIDIZI KUTOKA KWA MWENYEZI MUNGU

رَبَّنَآ اَخْرِجْنَا مِنْ هٰذِهِ الْقَرْيَةِ الظَّالِمِ اَهْلُهَا وَجْعَلْ لَّنَا مِنْ لَّدُنْكَ وَلِيًّا وَّجْعَلْ لَّنَا مِنْ لَّدُنْكَ نَصِيْرًا ۝

***Matamshi:*** *Rabbanaa Akh'rijnaa min haadhihil qaryati dhdhaalimi ahluhaa. Waj'allanaa minlladunka waliyyaa, waj'allana milladunka naswiiraa.*

**Tafsiri:** Mola wetu Ututoe katika mji huu ambao watu wake ni wadhalimu, na Utujaalie mlinzi kutoka Kwako, na Utujaalie msaidizi kutoka Kwako. (4:76).

## 27. DUA YA UPAMBANUO BAINA YA HAKI NA BATILI

**(Dua ya Nabii Shuaib a.s.)**

رَبَّنَا افْتَحْ بَيْنَنَا وَبَيْنَ قَوْمِنَا بِالْحَقِّ وَ اَنْتَ خَيْرُ الْفٰتِحِيْنَ ۞

***Matamshi:*** *Rabbana-ftah bainanaa wa baina Qauminaa bilhaqqi wa anta khairul faatihiin.*

**Tafsiri:** Mola wetu hukumu baina yetu na baina ya kaumu yetu kwa haki, nawe ndiwe Mbora wa wanaohukumu. (7:90).

## 28. DUA YA KUOKOLEWA NA WATU WADHALIMU

**(Dua ya watu wa Peponi).**

رَبَّنَا لاَ تَجْعَلْنَا مَعَ الْقَوْمِ الظّٰلِمِيْنَ ۞

***Matamshi:*** *Rabbanaa laa taj'alnaa ma'alqaumi dhdhaalimiin.*

**Tafsiri:** Mola wetu Usituweke pamoja na watu wadhalimu. (7:48).

رَبِّ نَجِّنِى مِنَ الْقَوْمِ الظّٰلِمِيْنَ ۞

***Matamshi:** Rabbi Najjinii minal qaumi dhdhaalimiin.*

**Tafsiri:** Mola wangu niokoe katika watu wadhalimu.(28:22).

## 29. DUA YA KUJIEPUSHA NA WADHALIMU

**(Dua ya Nabii Musa a.s.)**

رَبِّ فَلَا تَجْعَلْنِىْ فِى الْقَوْمِ الظّٰلِمِيْنَ ۞

***Matamshi:** Rabbi falaa taj'alnii Fil qaumi dhdhaalimiin*

**Tafsiri:** Mola wangu usinijaalie katika watu wadhalimu.(23:95).

## 30. DUA YA WOKOVU KATIKA HILA ZA WAPINZANI
**(Dua ya Nabii Luti a.s.)**

رَبِّ نَجِّنِيْ وَاَهْلِي مِمَّا يَعْمَلُوْنَ ۞

***Matamshi:*** *Rabbi Najjinii wa ahlii mimmaa yaamaluun.*

**Tafsiri:** Mola wangu, Uniokoe mimi na ahali zangu katika yale wanayoyafanya.(26:170).

## 31. DUA YA KUOMBA GHOFIRA BAADA YA KUKOSEA
**(Dua ya Nabii Musa a.s.)**

رَبِّ اِنِّيْ ظَلَمْتُ نَفْسِيْ فَاغْفِرْ لِيْ ۞

***Matamshi:*** *Rabbi Innii dhalamtu nafsii faghfir lii.*

**Tafsiri:** Mola wangu nimedhulumu nafsi yangu basi nighofirie.(28:17).

## 32. DUA YA KUOKOLEWA KATIKA FITINA YA MAKAFIRI NA WAFISADI

### A. (Dua ya watu wa Nabii Musa a.s.).

رَبَّنَا لاَ تَجۡعَلۡنَا فِتۡنَةً لِّلۡقَوۡمِ الظّٰلِمِيۡنَ ۞ وَنَجِّنَا بِرَحۡمَتِكَ مِنَ الۡقَوۡمِ الۡكٰفِرِيۡنَ ۞

***Matamshi:*** *Rabbanaa laa taj'alnaa fitnatan lilqaumi dhdhaalimiin wa najjinaa birahmatika minal qaumil kaafriin.*

**Tafsiri:** Mola wetu usitufanye jaribio kwa watu wadhalimu. Na Utuokoe kwa rehema Yako na watu wadhalimu.(10:86-87).

### B. (Dua ya Nabii Lut a.s.)

رَبِّ انۡصُرۡنِیۡ عَلَی الۡقَوۡمِ الۡمُفۡسِدِيۡنَ ۞

***Matamshi:*** *Rabbi n'swurnii Alal Qaumil mufsidiin.*

**Tafsiri:** Mola wangu unisaidie juu ya watu wafisadi. (29:31).

**C. (Dua ya Nabii Ibrahim a.s.).**

رَبَّنَا لَا تَجْعَلْنَا فِتْنَةً لِّلَّذِينَ كَفَرُوا وَاغْفِرْ لَنَا رَبَّنَا إِنَّكَ أَنتَ

الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ۝

***Matamshi:*** *Rabbanaa laa taj'alnaa fitnatan llilladhiina kafaruu waghfir lanaa Rabbanaa innaka antal Aziizul Hakiim.*

**Tafsiri:** Mola wetu, Usitufanye jaribio kwa wale waliokufuru, na Utughofiri, Mola wetu hakika Wewe ni mwenye nguvu, mwenye hekima.
(60:6).

## 33. DUA YA KUOMBA MSAADA WA MWENYEZI MUNGU

### A. (Dua ya Nabii Nuhu a.s.)

اَنِّىْ مَغْلُوْبٌ فَنْتَصِرْ ۞

***Matamshi:*** *Innii Maghluubun fantaswir*

**Tafsiri:** (Mola wangu) kwa hakika nimeshindwa basi nisaidie.(54:11).

### B. (Dua ya Nabii Nuhu a.s.)

رَبِّ انْصُرْنِىْ بِمَا كَذَّبُوْنِ ۞

***Matamshi:*** *Rabbin Swurnii bimaa kadhdhabuun.*

**Tafsiri:** Mola wangu unisaidie kwa sababu wamenikadhibisha.(23:27).

## 34. DUA YA MAANGAMIO YA MAKAFIRI

### A. (Dua ya Nabii Nuhu a.s.)

رَبِّ لَا تَذَرْ عَلَى الْاَرْضِ مِنَ الْكٰفِرِيْنَ دَيَّارًا ۝

***Matamshi:*** *Rabbi laa tadhar ala l'ardhi minal kaafiriina dayyaaraa.*

**Tafsiri:** Mola wangu usiache juu ya ardhi mkazi ye yote katika makafiri (71:27).

### B. (Dua ya Nabii Musa a.s.)

رَبَّنَا اطْمِسْ عَلٰٓى اَمْوَالِهِمْ وَاشْدُدْ عَلٰى قُلُوْبِهِمْ ۝

***Matamshi:*** *Rabbana tw'mis alaa am'waalihim wash'dud alaa quluubihim*

**Tafsiri:** Mola wetu, ziangamize mali zao na ishambulie mioyo yao. (10:89).

## 35. DUA YA KUOMBA WEMA KATIKA DUNIA NA AKHERA NA KUJIKINGA NA ADHABU YA MOTO

رَبَّنَآ اٰتِنَا فِى الدُّنْيَا حَسَنَةً وَّ فِى الْاٰخِرَةِ حَسَنَةً وَّقِنَا عَذَابَ النَّارِ ۝

**A.** ***Matamshi:*** *Rabbanaa aatinaa fii dduniya hasanatan wwafil aakhirati hasanatan wwaqinaa adhaaban naar.*

**Tafsiri:** Mola wetu utupe wema duniani na wema katika Akhera na Utulinde na adhabu ya Moto. (2:202).

رَبَّنَآ اِنَّنَآ اٰمَنَّا فَاغْفِرْ لَنَا ذُنُوْبَنَا وَقِنَا عَذَابَ النَّارِ ۝

**B.** ***Matamshi:*** *Rabbanaa innanaa aamanaa faghfir lanaa dhunuubanaa waqinaa adhaaban naar.*

**Tafsiri:** Mola wetu hakika sisi tumeamini, basi

utughofirie madhambi yetu, na Utuepushe na Adhabu ya Moto.(3:17).

رَبَّنَا مَا خَلَقْتَ هٰذَا بَاطِلاً سُبْحٰنَكَ فَقِنَا عَذَابَ النَّارِ ۝

**C. *Matamshi:*** *Rabbanaa maa khalaqta hadhaa baatwilan. Sub'haanaka faqinaa adhaaban naar.*

**Tafsiri:** Mola wetu Hukuviumba hivi bure; utukufu ni Wako, basi Utuepushe na adhabu ya Moto. (3:192).

رَبَّنَا اصْرِفْ عَنَّا عَذَابَ جَهَنَّمَ اِنَّ عَذَابَهَا كَانَ غَرَامًا ۝

**D. *Matamshi:*** *Rabbana-swrif 'annaa 'adhaaba Jahannama inna 'adhaabahaa kaana gharaamaa.*

**Tafsiri:** Mola wetu utuondolee adhabu ya Jahannam, bila shaka adhabu yake ndiyo iendeleayo. (25:66).

## 36. DUA YA KUPATA SUBIRA NA KIFO CHEMA
**(Dua ya wachawi waliomwamini Nabii Musa a.s.)**

رَبَّنَآ اَفۡرِغۡ عَلَيۡنَا صَبۡرًا وَّتَوَفَّنَا مُسۡلِمِيۡنَ ۞

***Matamshi:*** *Rabbanaa afrigh alainaa swabran wwatawaffanaa Muslimiin.*

**Tafsiri:** Mola Wetu tumiminie uvumilivu na Utufishe watii.(7:127).

## 37. DUA YA KUWA MTU MWEMA KUTAJWA KWA WEMA NA KUPATA PEPO
**(Dua ya Nabii Irahim a.s.)**

رَبِّ هَبۡ لِيۡ حُكۡمًا وَّاَلۡحِقۡنِيۡ بِالصّٰلِحِيۡنَ ۞ وَاجۡعَلۡ لِّيۡ لِسَانَ
صِدۡقٍ فِي الۡاٰخِرِيۡنَ ۞ وَاجۡعَلۡنِيۡ مِنۡ وَّرَثَةِ جَنَّةِ النَّعِيۡمِ ۞

***Matamshi:*** *Rabbi Hablii Hukman wwa alhiqnii bi sswaalihiin. Waj'allii lisaana swidiqin fil aakhiriin. Waj'allii min wwarathati jannatin-naiim.*

**Tafsiri:** Mola wangu Unipe (nguvu ya kutoa) hukumu na Uniunge pamoja na watendao wema. Na unijaalie kutajwa kwa wema katika watu wa baadaye. Na Unijaalie katika warithi wa Bustani za neema. (26:84-86).

## 38. DUA YA KUPATA WEMA KATIKA DUNIA NA AKHERA
**(Dua ya Nabii Musa a.s.).**

وَاكْتُبْ لَنَا فِىْ هٰذِهِ الدُّنْيَا حَسَنَةً وَّفِى الْاٰخِرَةِ اِنَّا هُدْنَآ اِلَيْكَ ۞

***Matamshi:*** *Waktublanaa fii haadhihii dduniyaa hasanatan wwa fil aakhirati, Innaa hudnaa Ilaika.*

**Tafsiri:** Na Utuandikie mema katika dunia hii na Akhera; bila shaka tumeelekea Kwako. (7:157).

## 39. DUA YA KUEPUSHWA KUOMBA JUU YA JAMBO USILO NA ELIMU NALO
**(Dua ya Nabii Nuhu a.s.)**

رَّبِّ اِنِّيِّ اَعُوْذُبِكَ اَنْ اَسْئَلَكَ مَا لَيْسَ لِىْ بِهٖ عِلْمٌ وَاِلَّا تَغْفِرْلِىْ
وَتَرْحَمْنِيِّ اَكُنْ مِّنَ الْخٰسِرِيْنَ ۞

**Matamshi:** *Rabbi innii a'uudhubika an as'alaka maa laisa lii bihii 'ilmun wwaillaa tadhfirlii watarhamnii akun mminal khaasiriin.*

**Tafsiri:** Mola wangu, hakika mimi najikinga Kwako nisije kukuomba nisiyoyajua; na kama Hutanisamehe na kunirehemu, nitakuwa miongoni mwa wapatao hasara. (11:48).

## 40. DUA YA KUJIKINGA KWA MWENYEZI MUNGU

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ۞

قُلْ اَعُوْذُ بِرَبِّ الْفَلَقِ ۞ مِنْ شَرِّ مَا خَلَقَ ۞ وَمِنْ شَرِّ غَاسِقٍ اِذَا
وَقَبَ ۞ وَمِنْ شَرِّ النَّفّٰثٰتِ فِى الْعُقَدِ ۞
وَمِنْ شَرِّ حَاسِدٍ اِذَا حَسَدَ ۞

**A.** ***Matamshi:*** *Bismillahir-Rahmaanir-Rahiim. Qul a'uudhu birabbil falaq. Min sharri maa khalaq, wamin sharri ghaasiqin idhaa waqab, wa min sharrin Naffaathaati fil 'uqad, wamin sharri haasidin idhaa hasad.*

**Tafsiri:** Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.
2. Sema: Najikinga kwa Mola wa mapambazuko,
3. (Anilinde) katika shari ya Alivyoviumba,

4. Na katika shari ya giza la usiku liingiapo,
5. Na katika shari ya wale wanaopulizia mafundoni,
6. Na katika shari ya hasidi anapohusudu.
(113:1-6).

بِسْمِ ا للّٰهِ الرَّ حْمٰنِ الرَّ حِيْمِ ۞
قُلْ اَعُوْذُ بِرَبِّ النَّاسِ ۞ مَلِكِ النَّاسِ ۞ اِلٰهِ النَّاسِ ۞
مِنْ شَرِّ الْوَسْوَاسِ الْخَنَّاسِ ۞
الَّذِىْ يُوَسْوِسُ فِىْ صُدُوْرِ النَّاسِ ۞ مِنَ الْجِنَّةِ وَالنَّاسِ ۞

**B.** ***Matamshi:*** *Bismillahir-Rahmaanir-Rahiim. Qul a'uudhu birabbin-Naas, Malikin-Naas, Ilaahin-Naas; min sharril was'waasil khannaas. Alladhii yuwas'wisu fii suduurin-Naas. Minal jinnati wan-Naas.*

**Tafsiri:** Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.
2. Sema: Ninajikinga kwa Mola wa watu,
3. Mfalme wa watu,

4. Mwabudiwa wa watu,
5. Katika shari ya wasiwasi wa (Shetani) aendaye kisirisiri kwa hila,
6. Atiaye wasiwasi mioyoni mwa watu,
7. Miongoni mwa majini na watu. (114:1-7).

# QURANIC PRAYERS

## Kiswahili Version

**By**

**Muzaffar Ahmad Durrani**

ISBN 9987-8932-1-x

Many Quranic Prayers have been compiled in this pocket book, to make it easy for our new readers. There is transliteration of Arabic text in Roman letters and its Kiswahili translation.
It has been also mentioned that certain prayer was used by which Prophet.

**AHMADIYYA MUSLIM JAMAAT TANZANIA**

لَآاِلٰهَ اِلَّا اللّٰهُ مُحَمَّدٌ رَّسُوْلُ اللّٰهِ

# اَدُعِيَّةُ القُرآنِ الكَرِيم

# MAOMBI

## YA

## QUR'AN TUKUFU

SHEIKH MUZAFFAR AHMAD DURRANI

# QURANIC PRAYERS

## Kiswahili Version

**By**

**Muzaffar Ahmad Durrani**

ISBN 9987-8932-1-X

Many Quranic Prayers have been compiled in this pocket book. To make it easy for our new readers, there is transliteration of Arabic text in Roman letters and its Kiswahili translation.
It has been also mentioned that certain prayers were used by particular Prophet.

**AHMADIYYA MUSLIM JAMAAT TANZANIA**